# Hebu Tusherehekee Mama



# Yaliyomo

Uwasilishaji.............................................. 2
Shughuli .................................................. 3-4
Mapambo ............................................. 5-6
Fungu la Maneno...................................... 7-8
Michezo.................................................... 11-12
Mashairi......................................................... 13-15
Maelekezo......................................................16
Mahubiri...................................................... 17-18
Programu.................................................... 18



## Uwasilishaji



Ni furaha yangu kukupa mawazo kadhaa ya jinsi ya kusherekea Siku ya Mama.
Pamoja tutapanga kuwa na wakati maalum na uliochaguliwa kwa makini ili kuwaheshimu mama zetu.

Kuanzisha mpango wa kusherehekea mama ni fursa nzuri sana ya kufanya kazi pamoja na timu yetu katika: michezo ya kuigiza, matukio maalum na watoto, kupamba kanisa, kuchangisha fedha, nk.

Furahia mawazo yafuatayo ili upate msingi wa shughuli bunifu katika kanisa lako na pamoja na watoto wako.

Maoni na hadithi zozote. Usisahau kutuandikia! Itakuwa baraka kukujua na kujifunza pamoja nawe.

Heri katika Siku ya Mama, Mama wa Guatemala!





Mavet

Maria Veronica Toj
Huduma ya Watoto ya Arcoíris y Los Niños Cuentan
mavet@losninoscuentan.com
Facebook: veronicatoj








## Shughuli

* Chagua neno bunifu kwa ajili ya shughuli yako: Malkia wa Sherehe, Ua Linalopendeza Zaidi, Mama wa Nguvu, nk.

* Pamba kila kitu kwa nyota za dhahabu. Inaweza kuwa siku ya manyota, unajua.

* Wanapowasili katika tukio, watendee kama malkia, na kuwavalisha taji za karatasi za kumetameta za kuandika majina yao.Mataji yanaweza pia kuwa ya plastiki na wanaweza kwenda nayo nyumbani.

* Mwishowe unaweza kutoa stashahada ya kuvutia na thawabu kwa washiriki wote.Tabasamu la kuvutia zaidi, mavazi mazuri, utani zaidi, upendo zaidi, mpenzi anaye enziwa zaidi, walioalikwa katika sherehe, nk.

* Kulala nje.Wazo nzuri la kushiriki kati ya wasichana na mama zao. Kila msichana anapaswa kumwalika mamake na kushiriki katika shughuli za kujifurahisha, mwishowe kulala katika mifuko ya kulala. Ikiwa mama yao hapatikani wanaweza kumwalika shangazi, rafiki, nk.

- Mpango wako unaweza kujumuisha: moto wa kuota, kutunza kucha za mikono, vinyago vya uso, sinema, vitafunio, hekaya za kusisimua, mashindano ya nyimbo (karaoke), nk.
-Unaweza kuwa na mashindano ya: nguo za kulala, sapatu, mitindo ya nywele, kuvaa sawa, nk. Unaweza kuandaa vizuri wakati wa chakula cha jioni ili kuwa wa kipekee kwao.
-Usahau kuwa na awamu ya mazungumzo ya sala kwa kina mama na wasichana. Unaweza kufunga kwa kifungua kinywa maalum, kabla ya Siku ya Mama.
* Unaweza kuwa na awamu ya kupiga picha ambapo watoto watavaa mavazi yanayokaribia kufanana ya mama

zao. Yatakavyolingana zaidi ndivyo itakuwa ya kupendeza




* Tengeneza tai za karatasi kwa watoto, fanya watoto kuzipamba wenyewe na kuwasubiri mama zao mlangoni, kama wagwana wa kweli wanavyowasubiri malkia.
* Unaweza kupanga kuwa watoto watavaa mavazi yanayofanana na ya mama zao.
* Jitayarishe na kufanya mazoezi pamoja na watoto, wazazi na watu wengine wa familia kwa ajili ya awamu maalum kama vile mashairi, mashindano, maonyesho ya michoro, michezo, nk, ili kushiriki kama familia.



* Shangaza Mama kwa kuchora picha zake bora ukutani.
* Tengeneza Eneo lililonandikwa Majina kwenye Sakafu katika sehemu fulani ya kanisa lako na kuweka picha au nyota na jina kamili la kila mama kwenye sakafu.



* Usisahau kwamba kuna watoto ambao mama zao hawajafika au wamefariki. (Kuwa na wakati wa kimya, na eneo maalum linaloitwa Mbinguni, na kuweka picha au michoro ya mawingu au nyota. Sehemu fulani ya kuweka ushuhuda kutoka kwa mwanamke ambaye ni wa muhimu katika maisha ya mtoto).



* Kumbuka kumshirikisha mke wa Mchungaji wa kanisa katika shughuli hii.
* Sherehekea kwa kutoa maua kwa mama mzee zaidi katika kanisa, mama aliye na watoto wengi, nk.
* Siku chache kabla unaweza kutumia kamera rahisi kurekodi salamu za watoto na kuzionyesha wakati wa sherehe.
* Katika tukio moja tulikusanya masanduku makubwa ya kadibodi na kuyaweka kama zawadi kwenye jukwaa.Kisha, tukawaarifu kina mama kwamba watoto wa chekechea walikuwa na zawadi. Watoto wanaingia ndani ya sanduku na linapofunguliwa wanatokea wakiwa na karatasi za muundo wa roho na wakikariri shairi.
ith paper hearts in their hands and saying a poem.





# Mapambo



*Tumia karatasi tupu kuunda ‘mifuko’ na kupamba kila kiti ambacho kina mama wataketi.

*Weka riboni ya rangi au taji ya karatasi ya dhahabu nyuma ya kila kiti.

* Puto ni vifaa vizuri vya kutumia kama mapambo. Changanya rangi tofauti na kuzipanga kwa muundo maalum. Pendekezo moja la muundo ni kutumia puto kutengeza maua.



## Maua ya Puto

Puliza puto ndefu hadi mwisho, na kuachilia hewa kidogo ili kuwa nyororo. Wazo ni kufanya puto kuonekana kama imepulizwa kabisa, lakini unaposukuma pande zote mbili unapaswa kuweza kushikanisha vidole bila tatizo lolote. Funga shingo la puto kwa kutumia upande ule mwingine wa mwisho ili kuunda pete.




Gawanya pete katika sehemu tatu sawa. Ukipinda na kuviringisha kila thuluthu mara mbili. Shika theluthi tatu katika muundo wa ‘Z’.




Sasa una pete tatu ndogo zilizounganishwa. Shika kila mwisho wa ‘Z’ (ncha A na B) na kusukuma katikati. Sasa sehemu ya katikati ‘soseji’ (ncha C) inaunda ‘vilele’ cha petali.



Kisha pinda ili kushikanisha petali. Sehemu hii ni ngumu kidogo, tunapaswa kulazimisha puto kidogo. Hivyo mipindo itakuwa imefichwa, na tutapata petali sita laini.




Kwa ajili ya shina, puliza puto la kijani, aina ya 260 au 160 na kuingiza mwisho ulio laini (sio kifundo) kupitia katikati

ya petali (hadi kufika katikati).
Gawanya puto za kijani zilizobaki katika tatu, na kuziunda kama ‘Z’.



Kuchukua matawi matatu kwa pamoja, na kupinda kwa nusu.




Hii huunda majani mawili na shina.

Sasa, weka ua katika chombo kizuri cha maua!



*Mioyo inayoning’inia

Unachohitaji ni yafuatayo:

- Kadibodi katika rangi ambazo unapenda
- Mkasi
- Mioyo ya Udongo wa Mboji
- Kalamu za kuweka alama
- Uzi wa uvuvi



Tumia mioyo ya udongo wa mboji kuchora maumbo tofauti kwa kalamu za kuweka alama. Kata na ugawanye. Tumia maumbo yaliyo sahihi, kama inavyoonyeshwa.
Hatimaye, tunapaswa kuweka mioyo iliyokatwa katika uzi wa uvuvi katika mstari wa wima, uzi mmoja chini ya mwingine. Ikiwa tunataka kupendeza zaidi, tunaweza kubadilisha ukubwa na rangi ya mioyo ili kufanya ipendeze zaidi.





* Unaweza kutumia bendera zilizotengenezwa kwa vitambaa vya rangi yoyote au rangi zote.



## Fungu la Maneno

- Inapofika ni kupenda, 'Mama' ni neno linalofaa. Asiyejulikana

- Mama huelewa kile mtoto hasemi. Methali ya Kiyahudi

- Mama ni mtu ambaye akigundua kuna vipande vinne tu vya keki na kuna watu watano, anatangaza na kusema kuwa haipendi keki. Tenneva Jordan

- Mtu fulani aliuliza msichana nyumbani kwao ni wapi, alijibu, 'ambapo mamangu yupo. 'Keith L. Brooks

- Katika sikio la mtoto, neno 'mama' ndilo la kuvutia zaidi kwa lugha yoyote. Arlene Benedicto XVI

- Moja ya mahitaji makubwa ya mwanadamu ni kuwa mtu anayejali ulipo? unapokosa kurudi nyumbani usiku. Margaret Mead

- Kila mara mama huwaza mara mbili, moja kwa ajili yake na moja kwa ajili ya mwanawe, kwa ajili yake na ya mwanawe.Kwa ajili yake na ya mwanawe. Sophia Loren

- Jinsi nilivyo ni kwa ajili ya mamangu.Mafanikio yangu yote katika maisha imetokana na mafundisho ya kimaadili, kiakili na kimwili niliyopokea kutoka kwa mama. George Washington

- Nakumbuka sala alizofanya mamangu na zinanifuata hadi leo. Zimekuwa sehemu yangu maisha yangu yote. Abraham Lincoln

- Upendo wa mama ni amani.Sio kitu cha kutafuta, wakati mwingine hatustahili. Erich Fromm

- Mama hupenda wanawe, hata kama hawastahili kupendwa. Kate Samperi

- Mamangu alikuwa na mwili mwembamba, na mdogo,



lakini moyo mkubwa - moyo mkubwa kiasi kwamba furaha ya kila mtu ilijihisi nyumbani ndani yake, na ukarimu. Mark Twain

- Nampenda mamangu jinsi mti unavyopenda maji na jua - hunisaidia kunawiri, kufanikiwa, na kufikia mambo makubwa. Terri Guillemets

- Maisha ilianza kwa kuamka na kuupenda uso wa mama yangu. George Elliot

- Mama anaweza kuchukua nafasi ya wengine wote lakini hakuna anayeweza kuchukua nafasi yake. Kardinali Mermillod

- Wanawake wote huwa kama mama zao.Inashangaza. Hakuna mwanamume anayeweza kufanya hivyo. Oscar Wilde

- Kuwa mama wakati wote ni mojawapo ya kazi yenye malipo ya juu zaidi katika sekta yangu, maana malipo yake ni upendo halisi. Mildred B. Vermont

- Kati ya haki zote za wanawake, iliyo ya muhimu zaidi ni kuwa mama. Lin Yutang

- Ninamshukuru Baba wa milele, si kwa sababu aliwaumba wa kuvutia, bali kwa sababu alimpa kila mmoja moyo wa kuwa mama. José Hernández

- Jinsi nilivyo na ninavyotumai kuwa, ni kwa ajili ya marehemu mama yangu.Hakuna mtu anayeweza kuwa maskini ikiwa mamake ni mwanamke wa imani. Abraham Lincoln.

- Mama ni jina la Mungu katika nyoyo na midomo ya watoto. William Thackeray

- Nieleze kuhusu uso wa mama yako na nitakueleza wewe ni nani. Khalil Gibran



# Michezo



* *Kina Mama wa Watu Maarufu*

Kusanya vipande vya picha vya waigizaji, waimbaji, wanasiasa na wachoraji, nk., vya watu maarufu. Unaweza kucheza katika makundi au mama kwa watoto, toa picha tofauti kwa kila kikundi. Wanapopokea picha hio, wanapaswa kuandika nini mama wa mhusika huo anaweza kusema ikiwa angeiona picha hiyo sasa.Kisha, watashiriki na kila mtu picha hio na yale waliyoandika.

* *Kubahatisha ni mboga gani*



Chukua matunda na mboga kadhaa za kila aina na kuzifunga kwa vibamba ili kupata umbo. Ziweke katika sanduku na funika macho ya kina mama kwa kitambaa. Mchezo huu unaweza kuchezwa kama timu tofauti.Wengine wanaanza, wanaweka mikono yao ndani ya sanduku, wanachukua mboga na wanapaswa kukisia ni mboga gani.Wanapaswa kuwa na nafasi moja tu. Ikiwa huwatakisia, timu inayofuata inashinda.Timu inakisia mboga zaidi wanashinda. Unaweza kufanya mchezo kuwa mgumu, kwa mfano, kuuliza kile mboga hiyo hutumiwa kupika.Au, kile wanaweza kutumia kupika badala ya mboga hio, nk?

* *Taji la Malkia*



Chora malkia mkubwa bila taji, bila fimbo na bila koti. Tindika kwenye ukuta kwa urefu ambao kila mtu anaweza kufikia juu ya picha. Mchezo unahusisha kina mama, wamefungwa macho kwa kitambaa na wanapaswa kuweka sehemu zinazokosa katika sehemu sahihi kwenye picha. Kila sehemu wanayoweka inapaswa kuwa na gundi ili kushika.

* *Simama - Keti!*

Patia kila mshiriki namba (washiriki kadhaa wanaweza kuwa na namba sawa). Kisha eleza hadithi ya utani

inayojumuisha namba nyingi, na mtu au watu walio na namba hiyo wanapaswa kusimama. Eleza hadithi kwa kasi na kuongeza kasi kila awamu.




* *Maneno yanayokosa*

Baada ya kufanya makaribisho cheza mchezo huu: chini ya dakika 3 unapaswa kupata, mama na wanawe, maneno mengi yaliyofichwa katika: 'Siku ya Mama yenye Furaha' (raha, sifu, sima, nk) Timu inayoandika maneno zaidi inakuwa washindi. (Tayarisha zawadi kumi)

* *Nyota*

Unahitaji kuchora nyota kadhaa za rangi kwenye sakafu ya chumba, unaweza kutengeneza kwa utepe au kutoka kwa karatasi. Baadhi ya nyota zinapaswa kuwa kubwa kiasi kwamba watu wawili wanaweza kutoshea ndani, zingine za watu wanne, nk. Tengeneza nyota chache kuliko idadi ya watu. Weka alama ya kuonyesha sehemu ya kuondoka. Unapotoa ishara, kina mama wote wanaenda na kutafuta nyota ya kusimama ndani, kabla hujasema: Tosha.



Washiriki wote wanapaswa kubaki wamesimama na bila kusonga, ikiwa wanagusa kingo moja ya nyota au mguu mmoja unatoka nje, wanaondoka.

Kama mchezo wa viti, unaweza kuondoa nyota ili kuongeza ugumu katika mchezo. Unaweza pia kucheza hadi kupata mshindi ambaye atakuwa nyota wa mchezo.



# Ufundi










## *Kitabu cha Mapishi

Haya si maelekezo ya kawaida na watoto watayaandika wao wenyewe. Wanapaswa kuandika jinsi wanavyoelewa, na kuamini kile mama zao hutumiakutengeneza chakula wanachopenda. Itakuwa ya kufurahisha kushuhudia watoto wakielezea mawazo yao kuhusu chakula cha Mama. Tumia majani ya rangi na majalada ya kupendeza.

* Unaweza kuleta lapulapu za rangi moja na kuwafanya watoto kuzipamba kwa kugandisha vifaa na kuchora kwa herufi. Zinaweza kuwa: makombe ya bahari, pinde za rangi, pamba za nguo, vipande vya kitambaa gandamizo, nk. Unaweza pia kufanya hivyo kwa kuchora herufu katika vikombe vyeupe au kupaka rangi maalum kwenye vyombo vya kauri.

## *Maua kwa Mama

Viungo:

-Chokoleti za rangi na ukubwa mbalimbali: ukubwa mdogo kwa ajili ya katikati.

-Nyeupe na za waridi kwa ajili ya petali za ukubwa wa kawaida.

-Glasi ya sukari ya muundo wa Triple A na matone ya maji kwa ajili ya gundi.

-Vijiti vya mshikaki - Mifuko ya karatasi za selofeni

-Utepe wa kupamba

Maelekezo: Tayarisha gundi katika glasi iliyo na sukari kiasi kidogo na majone machache ya maji.Koroga kwa kijiko mpaka ianze kunata. Ongeza matone ya maji ikiwa inafaa au sukari zaidi ikiwa gundi yako ni nyepesi sana. (Unaweza pia kununua katika duka la kuoka).Weka ncha ya kijiti katika maji. Kisha ingiza kwenye pipi ya kawaida mpaka ufikie upande ule mwingine wa pipi, kisha weka chokoleti ndogo katika sehemu ya katikati.Weka gundi kidogo katika sehemu zinapoungana. Una msingi wa picha yako. Kisha weka chokoleti katika upande wa kulia na wa kushoto ili kutengeneza ua na kugandisha. Acha ikauke na kisha kuiweka katika mfuko wa selofeni na kufunga kwa riboni ya rangi unayopenda.

## *Mfuko wa chokoleti







Vifaa

- Vitambaa na nyuzi zozote - Chokoleti ndogo ndogo
- Karatasi yoyote ya zawadi

Tumia vitambaa vya kawaida. Kata ukubwa unayotaka na kuzingatia nafasi ya juu utakapotumia kufunga kikapu na utepe wa juu.Andika maandishi yatakayopambwa kwa penseli na kufanya michoro kwenye herufi. Shona pande na kufunga mfuko kwa utepe. Kwa chokoleti, ondoa karatasi ya juu na kuandika maneno ya upendo katika karatasi ya ndani. Pakia tena. Weka ndani ya mfuko na kwa hakika mama atakuwa akijawa na mshangao kila wakati anakula chokoleti.



## *Maua iliyo na karameli

Bao za kubebea Pipi zilizowekwa kwenye karatasi za umbo wa moyo.Tumia kiasi kidogo cha gundi na kwa dakika chache utakuwa na shada la maua la kupendeza. Unaweza kutengeneza kwa kuziweka kwenye chungu kidogo, au kutengeneza shada la maua kutoka kwa karatasi ya rangi.



## *Kikaragosi aliyejawa na upendo



Unahitaji:

- Kadibodi ya rangi yoyote - Kifaa cha kutengeneza mashimo
- Mkasi
- Kalamu za kuweka alama - Gundi - Macho inayosonga na kunata

Utaratibu: Kata umbo la moyo kutoka kwa kadibodi na kutengeneza shimo kwa ajili ya kila kidole katika upande wa chini wa umbo (vidole vinapaswa kuingia bila tatizo ).Pamba umbo la moyo kwa kalamu za alama, na kuchora viungo vya uso na kuandika ujumbe nyuma yake.Kisha, gandisha macho ya kusonga na kuwahimiza watoto kuandika jumbe za upendo kwa Mama.

## *Vioo vilivyopambwa



Kitu ambacho Mama hawezi kupinga ni kujiangalia kwenye kioo. Vioo huja kwa ukubwa na maumbo tofauti. Unaweza kuleta vifaa mbalimbali ili watoto watumie kupamba. Vinaweza kuwa makoa ya bahari, mchanga, ndoano za nguo, vijiti vya mbao, riboni, vifungo, karatasi, vifuniko vya plastiki, karatasi, stika, nk.

# Mashairi



*Nguo safi
Niliumbusu mkono wake, nikahisi harufu ya sabuni:
Wangu niliubeba kando ya moyo.
Mkono wake niliumbusu kwa ufupi na kwa upole
Na kinywa changu kilijawa na manukato.
Msichana msafi, nani awezaye kukutisha,
Mikono yanukia sawa na nguo mpya.
Nilizimbusu nywele zake zake ndefu:
Na zilinukia kama nguo safi!
Unaoshea wapi mwili na mavazi yako?
Ni kisimi kipi unaoshea uso wako?
Msichana mdogo msafi, ungekuwa kinywaji
Kilichojaa maji safi. _Luis Cardoza and Aragón




*Mamita
Mamita, mamita tazama jinsi unavyopendeza,
Ukiyatizama maua haya bintiyo anakupa.
Tabasamu, mamita mrembo,
Macho yangu yanavutwa na uso wako unaong'aa,
Unafanana na binti mfalme, binti mfalme halisi
Umevaa kama rafiki, mama mtamu.
Mama, neno bora zaidi.
Kwa ushupavu nasema kuwa neno mama ndilo bora zaidi
Kwa sababu simwambii tu mtu
aliyenipa uhai, lakini aliyejinyima
Ili nipate maisha, katika siku alizokosa usingizi
Kwangu nuru haikukosa.
Ndilo neno bora zaidi nililotamka
Nilipopata mambo hayakuwa jinsi nilivyotarajia.
Naomba tu kuwa neno hili halitafutwa kutoka kumbukumbu yangu
Neno hilo ambalo sitaki kusahau kamwe. _Asiyejulikana

*Shairi lililopangwa kialfabeti kwa mama (Mama)

**M**ama ni wa kuvutia na wa kipekee
**A**najali na ni wa ajabu;
**M**makinifu katika maneno yake ya kila siku
**A**nifanya nitamani kujifunza hekima yake.
... -Asiyejulikana

*Zawadi ya "Siku ya Mama"

Mama wa kupendeza,
Mama mzuri
Leo hii, siku hii
Kwa hisia nzuri;
Nimefika kukuambia
Nakupenda sana
Na kukupa sadaka
na wimbo huu;
Niliomba mbingu,
Inipe nyota nyeupe,
Kwa mashamba ya kijani,
Nikaomba ua.
Katika usiku mtulivu,
Miale ya mwezi
Kwa bahari nataka lulu
Na trilioni kutoka kwa shomoro.
Nilipopata kila kitu,
Najiunga nawe kwa busu,
Sina kingine
Na ndicho nitakupa.
Natakifunga kwa upinde
Wa upendo
Na ndani, kitovuni...
Moyo wangu wakukarib-
ia!
-Asiyejulikana





*Umeniunganisha

Umeniunganisha tumboni
Katika tumbo la mamangu
Nakushukuru, nakushukuru
Umeniunganisha ndani yako mama
Kazi zako ni za ajabu//
Nakushukuru //
Umeniunganisha ndani ya mama yangu.
Umeniunganisha tumboni
Katika tumbo la mamangu
Nakushukuru, nakushukuru
Umeniunganisha ndani ya mama yangu.
-Steve Green

Pendekezo:

Mashairi kama haya au yaliyoandikwa na watoto, yanaweza kuchapishwa na kukunja karatasi na kuweka kwenye sahani iliyopambwa na kuwapa kina mama wanapowasili kwenye tukio lako. Sahani moja na shairi moja kwa kila mtoto.



# Maelekezo

## * Soseji na Spageti

Pasta haijapikwa 'inawekwa' katika soseji kwa makini na kisha kupikwa kwa njia ya kawaida.

## * Mayai yaliyopikwa katika umbo la moyo

1) Pika yai.
2) Toa magamba ya yai na kufuata hatua zilizoonyeshwa kwenye picha hapa chini na kushikilia kijiti kwa ambo mbili mpaka likauke na kuwa na umbo.
3) Kata katika vipande viwili au zaidi na kugawa. Linaweza kutumika wakati wa kiamsha kinywa au pamoja na

spageti.

## * Matunda ya furaha

Kata tikiji maji kwa maumbo kama haya kwa kutumia kifaa hiki cha kukata cha umbo la nyota ama maumbo mengi halisi.Chagua kipande cha tunda, linapendekezwa bila mbegu, kata mduara kutoka upande hadi mwingine, na kuhakikisha umekata umbo vizuri. Kisha panga na kugawa kwa muundo wa kupendeza kwenye trei na kuweka vijiti vya kulia kuwezesha kula vipande. Utawaweza kwa hii! (Unaweza kutumia matunda mengine)















# Mahubiri

## Wito wa Mama

**Utangulizin:**

Nimechoka! Kazi ya mama sio rahisi! Naelewa watoto wangu, lakini nani wa kunielewa? Je, kuna mwongozo wa kusaidia mama katika kazi yake? Kina mama hujiuliza maswali haya kila siku.Kazi yao si rahisi na wakati mwingine inavunja moyo. Hebu tukumbuke wito wa Maria, mamake Yesu, aliyojifunza kutoka kazi yake kama mama, tunaweza kuutumia siku ya leo.

## Matatizo yaliyomkabili Maria

**1. Sifa mbaya.** Alipata mimba ya nje ya ndoa na aliishi katika mji mdogo. Labda katika maisha yako ya zamani kuna hali ambazo unaskia aibu na hatia. 2 Wakorintho 5:17.

**2. Umaskini.** Mary alijifungua katika hori. Sote tunapitia wakati mgumu lakini upendo huwa bure. Jipende mwenyewe, penda watoto wako, mpenzio na, zaidi ya yote, mpende Mungu. Marko 12:30.

**3. Mwana wa Maria alidharauliwa.** Mathayo 2:13 Hawakumchukia tu mtoto wao ... walitaka kumwua. Siku hizi watoto bado wanateswa na Shetani kwa sababu anataka kuiba urithi wako. Zaburi 127: 3

Hupaswi tu kuwalinda watoto wako, pia unastahili kuwafundisha jinsi ya kujilinda.

**4. Kupoteza mpendwa.** Yohana 19:25. Isaya 41:10.



**5. Rasilimali alizokuwa nazo Maria:**

* Luka 1:30. Mwanamke aliyejawa na neema.
* Luka 1: 38. Mwanamke aliyejitolea

* Luka 1: 42. Alikuwa na rafiki aliyemdhamini.
1 Wathesalonike 5:11

**Hitimisho:**
Kazi aliyoifanya Maria haikuwa rahisi. Ilisababisha shida nyingi, lakini matokeo yake yanadhihirika katika mwanawe: Mwokozi wa Dunia. Na ingawa mimi na wewe hatukujifungua Mwokozi wa Dunia, Mungu ana mipango mikuu juu ya maisha yetu. Na kama Maria, inastahili jitihada na kazi yetu.





## Programu

1. Karibu
2. Fanya watu kujuana kwa njia ya kufurahisha
3. Shughuli maalum
4. Mahubiri
5. Maombi kwa ajili ya kina Mama
6. Mashairi
7. Mashindano au michezo inayotuzwa
8. Utoaji wa Stashahada
9. Utoaji wa kazi zilizofanywa na watoto
10. Chakula
11. Kufunga




- -Tamasha
- -Maelezo
- -Matukio
- -Vifaa
- -Habari
- -Tuzo
- - Marafiki na zaidi!

20160

www.ChildrenAreImportant.com
info@childrenareimportant.com
We are located in Mexico.
00-52-592-924-9041